UNITED NATIONS CONFERENCE ON TRADE AND DEVELOPMENT
CONFÉRENCE DES NATIONS UNIES SUR LE COMMERCE ET LE DÉVELOPPEMENT

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**EMBAGO**

Yaliyomo katika taarifa hii kwa vyombo vya habari na ripoti inayohusiana nayo hayapaswi kunukuliwa au kufupishwa katika machapisho, matangazo au vyombo vya habari vya kielektroniki kabla ya tarehe **16 Agosti 2023, saa 3 asubuhi London**

**(11 asubuhi New York, 5 asubuhi Geneva, 6 mchana Nairobi)**

UNCTAD/PRESS/PR/2023/015*
*Asili: Kiingereza*

## RIPOTI YA UNCTAD: KUINUKA KWA AFRIKA KAMA NGUVU YA UGAVI DUNIANI

### Kutokana na rasilimali nyingi na soko la wateja linalokua, Afrika inaweza kuwa kivutio maarufu cha utengenezaji wa tasnia zinazotumia teknolojia kubwa na kiungo muhimu katika minyororo ya ugavi duniani.

*Geneva, 16 August 2023* - Nchi za Kiafrika zinaweza kuwa washiriki wakuu katika minyororo ya ugavi duniani kwa kutumia rasilimali zao kubwa za nyenzo zinazohitajika na sekta za teknolojia ya juu na soko lao la wateja linalokua, Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD) limesema katika Ripoti yake ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika 2023 iliyozinduliwa leo jijini Nairobi.

Minyororo ya ugavi inajumuisha mifumo na rasilimali zinazohitajika kuendeleza, kuzalisha na kusafirisha bidhaa na huduma kutoka kwa wasambazaji hadi kwa wateja.

"Huu ni wakati wa Afrika kuimarisha nafasi yake katika minyororo ya ugavi duniani huku juhudi za ugawaji bidhaa zikiendelea. Pia ni fursa kwa bara la Afrika kuimarisha viwanda vinavyoibuka, kukuza uchumi na kutengeneza ajira kwa mamilioni ya watu wake," Katibu Mkuu wa UNCTAD Rebeca Grynspan amesema.

Wingi wa madini na vyuma muhimu barani Afrika, zikiwemo alumini, kobalti, shaba, lithiamu na manganisi, vipengele muhimu katika tasnia zinazotumia teknolojia kubwa, unaliweka bara hili kama kivutio kwa viwanda, kwa sababu misukosuko ya hivi majuzi iliyosababishwa na mtikisiko wa biashara, matukio ya kijiografia na kutokuwa na uhakika wa kiuchumi zinalazimisha wazalishaji kugawanya maeneo yao ya uzalishaji.

Afrika pia inatoa faida kama vile ufikiaji mfupi na rahisi zaidi wa pembejeo za msingi, nguvu kazi ya vijana, inayofahamu teknolojia, na inayoweza kubadilika, na tabaka la kati linalokua na linalojulikana kwa kuendelea kuhitaji bidhaa na huduma za hali ya juu zaidi.

***Mawasiliano:** Kitengo cha Mawasiliano na Habari cha UNCTAD, +41 22 917 5549, +41 79 502 43 11, catherine.huissoud@unctad.org, http://unctad.org/press

Ili kupokea nyenzo zetu za vyombo vya habari, tafadhali jisajili kwa: http://unctad.org/en/Pages/RegisterJournalist.aspx.

**Kuimarisha minyororo ya ugavi barani Afrika ni muhimu kwa ukuaji wa kanda**

Ripoti hiyo inaangazia kwamba kuunda mazingira yanayofaa kwa viwanda vinavyotumia teknolojia kubwa kutasaidia kuongeza mishahara katika bara hilo, ambayo kwa sasa imewekewa kima cha chini cha dola 220 kwa mwezi, ikilinganishwa na wastani wa dola 668 katika bara la Amerika.

Ushirikiano wa kina katika minyororo ya ugavi wa kimataifa pia utaleta mseto katika chumi za Kiafrika, na kuongeza ustahimilivu wao kwa majanga yajayo.

Kupanua minyororo ya usambazaji wa nishati barani Afrika pia ni fursa ya kuharakisha hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Uwezo mkubwa wa nishati mbadala wa bara hili, hasa katika nishati ya jua, unaweza kusaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nishati vinavyotokana na mafuta.

Afrika inahitaji uwekezaji zaidi katika nishati mbadala ili kusaidia kuziba pengo kubwa la uwekezaji na kukabiliana na vikwazo vingine kwenye utengenezaji wa paneli za miale ya jua barani humo. Hivi sasa, ni takribani 2% tu ya uwekezaji wa kimataifa katika nishati mbadala inayoenda Afrika. Ukuaji wa uwekezaji katika nishati mbadala, kama ilivyoonyeshwa na UNCTAD, unaweza kukuza utengenezaji wa paneli za jua barani Afrika.

Kwa mfano, mwaka wa 2022, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ilikuwa mzalishaji mkubwa zaidi wa shaba barani Afrika, ikiwa na tani milioni 1.8 za metriki – na zaidi ya uchunguzi na uchimbaji, nchi hiyo inaweza kuwa mahali pazuri pa kusafisha bidhaa za chuma kwa tasnia ya magari ya umeme.

**Fungua fursa za mnyororo wa usambazaji wa Afrika: Wekeza katika miundombinu, teknolojia na ufadhili**

Afrika inahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu ili kuimarisha nafasi yake kama kituo cha ugavi.

Nchi 17 za Afrika, zikiwemo Angola, Botswana, Ghana na Afrika Kusini, tayari zimetekeleza kanuni za maudhui ya ndani ili kusaidia ukuaji wa minyororo ya ugavi wa ndani, kukuza uhamishaji wa teknolojia, kuunda nafasi za kazi na kuongeza thamani ndani ya mipaka yao.

Zaidi ya hayo, nchi za Afrika zinapaswa kupata kandarasi bora za uchimbaji madini na leseni za uchunguzi wa vyuma vinavyotumika katika bidhaa za teknolojia ya juu na minyororo ya usambazaji. Hii itaimarisha viwanda vya ndani na kuwezesha makampuni ya ndani kubuni, kununua, kutengeneza na kusambaza vipengele muhimu.

Utumiaji wa teknolojia za kibunifu za kidijitali pia ni muhimu katika kuboresha michakato ya ugavi. Nchi kama vile Kenya zimepata maendeleo makubwa katika nyanja hii, na viwango vya juu vya utumiaji wa ujuzi wa kidijitali barani Afrika.

UNCTAD inazitaka serikali kuunda sera nzuri, kukuza mazingira wezeshi ya udhibiti na kuongeza programu ili kukuza utumiaji mkubwa wa teknolojia hizi.

Shirika hilo la biashara na maendeleo la Umoja wa Mataifa pia linasisitiza wito wake wa suluhu bora za ufadhili ili kuzipa nchi na biashara za Kiafrika mtaji na ukwasi wa bei nafuu ili kuwekeza katika kuimarisha minyororo yao ya ugavi.

**Fedha zaidi za ugavi kwa biashara ndogo ndogo**

Ripoti hiyo inasema biashara ndogo ndogo na za kati za Kiafrika zinahitaji fedha zaidi za ugavi, ambazo zitaziba pengo la muda wa malipo kati ya wanunuzi na wauzaji, zitaboresha upatikanaji wa mitaji ya kufanya kazi na kupunguza matatizo ya kifedha.

Kulingana na ripoti hiyo, thamani ya kifedha ya soko la ugavi barani Afrika ilipanda kwa 40% kati ya 2021 na 2022, na kufika dola bilioni 41. Lakini hii haitoshi.

Bara hilo linaweza kukusanya fedha zaidi kwa kuondoa vizuizi vya ufadhili wa ugavi, ikiwa ni pamoja na changamoto za udhibiti, mtazamo wa hatari kubwa, na taarifa zisizotosheleza za mikopo.

UNCTAD pia inasisitiza haja ya msamaha wa madeni ili kuzipa nchi za Afrika nafasi ya kifedha ya kuwekeza katika kuimarisha minyororo yao ya ugavi, kwani kwa wastani zinalipa mara nne zaidi kwa kukopa kuliko Marekani na mara nane zaidi ya chumi za Ulaya.

-----------------------------------------------------

**Kuhusu UNCTAD**

UNCTAD ni shirika la biashara na maendeleo la Umoja wa Mataifa. Inasaidia nchi zinazoendelea kufikia manufaa ya uchumi wa utandawazi kwa haki na kwa ufanisi zaidi na kuziwezesha kukabiliana na vikwazo vinavyoweza kutokana na ushirikiano mkubwa wa kiuchumi.

Inatoa uchambuzi, inawezesha ujenzi wa maelewano na inatoa usaidizi wa kiufundi kusaidia nchi zinazoendelea kutumia biashara, uwekezaji, fedha na teknolojia kama njia za maendeleo jumuishi na endelevu.